

SHERIA YA ARDHI
NAMBA 4 YA MWAKA 1999

MKATABA WA KUPANGISHA BOHARI

KATI YA

CRISPIN MUTABUZI MUSHUMBUSI

NA

BUFFALO BICYCLE TANZANIA

**MKATABA WA KUPANGISHA BOHARI (450 sqm) NA OFISI (140 sqm) - MIKOCHENI-
LIGHT INDUSTRIAL AREA
KITALU NO. 47 MANISPAA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM.**

MKATABA WA UPANGISHWAJI WA BOHARI NA OFISI

Mkataba huu umetiwa saini leo tarehe ya mwezi2024.

Kati ya

CRISPIN MUTABUZI MUSHUMBUSI wa sanduku la Posta 25475, Dar es Saaam Tanzania (hapa akijulikana kama "**Mwenye Bohari**") ambaye hapa itawajumuisha kama itakavyoonekana na itakavyojulikana itawahusisha vile vile warithi na wahusika wote wa **Mwenye Bohari** kwa upande mmoja;

Na

BUFFALO BICYCLE TANZANIA wa sanduku la Posta 72015 Dar es Salaam, Tanzania (hapa akijulikana kama "**Mpangaji**") ambaye hapa itawajumuisha kama itakavyoonekana na itakavyojulikana itawahusisha vile vile warithi na wahusika wote wa **Mpangaji** kwa upande wa pili.

1.0 MKATABA HUU UNASHUHUDIA;

KWAMBA *Mwenye Bohari* ni mmiliki halali wa Kiwanja chenye Bohari na ofisi, kinachopangishwa kilichoko eneo la Mikocheni-Light Industrial Area, Kitalu No. 47, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam – Tanzania chenye bohari yenye ukubwa wa 450sqm, na ofisi zenye ukubwa wa 140 sqm.

KWAMBA *Mpangaji* ni kampuni, ambayo inategemea kupanga Kiwanja kilichotajwa kwenye Mkataba huu kwa ajili ya shughuli zake mbalimbali;

2.0 WAHUSIKA HAPA WANAKUBALIANA KUWA:-

2.1 Mkataba huu utakuwa wa miezi sita (6) baada ya muda huo kuisha mkataba huu unaweza kuongezwa endapo makubaliano yataridhiwa na pande zote mbili husika;


2.2 Mkataba huu utaanza rasmi tarehemwezi wa mwaka 2024.

- 2.3 Malipo ya kodi ya pango yatakuwa ni **Shilingi za Kitanzania Milioni Nane na Laki Moja (TZS. 8,100,000.00)** tu kwa mwezi; ambapo **Mpangaji** atatakiwa kumlipa **Mwenye Bohari** malipo ya kodi ya Bohari na ofisi hizo, ya miezi sita kwa pamoja kwa mara moja ambayo ni **Shilingi za Kitanzania Milioni Arobaini na Nane na Laki Sita (TZS 48,600,000)**.
- 2.4 Malipo ya kodi hiyo yatafanyika katika akaunti ya Mwenye Bohari yenye jina **CRISPIN MUTABUZI MUSHUMBUSI** iliyopo Benki ya **CRDB** yenye namba **0152395749700**.
- 2.5 Malipo ya kodi ya Bohari na ofisi yanayotajwa katika mkataba huu hayajahusisha kodi zozote za serikali. Ni malipo ya matumizi ya Bohari na ofisi pekee. Kodi zozote za serikali zinazohusisha mkataba huu zitalipwa na mpangaji.
- 2.6 Malipio ya kodi yanayotajwa katika mkataba huu, yatalipwa kabla ya mpangaji kuanza kutumia bohari na ofisi zinazopangishwa katika mkataba huu. Mkataba huu utaanza rasmi mara baada ya mpangaji kulipia gharama za upangishaji, zinazotajwa katika mkataba huu.
- 2.7 **Mpangaji** katika mkataba huu, anakubali kusubiria mpangaji aliyekuwepo sasa katika bohari, ahamishe mizigo yake,ndipo yeye aanze kutumia Bohari. Na endapo itatokea, mpangaji atahitaji kutumia bohari kabla ya mpangaji anayemaliza muda kutoa vitu vyake, mpangaji anakubali kubadilishiwa bohari na kupewa eneo lingine tofauti na eneo linaongelewa kwenye mkataba huu, mpaka pale mpangaji anayemaliza muda wake atakapotoka.
- 2.8 **Mpangaji** atatumia Bohari na ofisi katika hali ya usafi kwa kipindi chote cha mkataba huu na atakapomaliza mkataba wake atakabidhi Bohari na ofisitajwa hapo juu kama ilivyokuwa siku ya makabidhiano;
- 2.9 **Mpangaji** atatakiwa Kuwa mstari wa mbele kutoa taarifa muhimu endapo utahisi kuna hali yoyote isiyo ya usalama katika mazingira yanayokuzunguka. Hii ni kwa faida ya mpangaji pamoja na wale wote walio jirani.
- 2.10 **Mpangaji** atatakiwa kulipa bili za matumizi ya maji na umeme kwa wakati kwa kipindi chote atakachokuwa anatumia Bohari na ofisi tajwa katika mkataba huu.

- 4.4 Jambo lolote lililotokea katika mkataba huu au linalohusu mkataba huu litakuwa linaongozwa na kutafsiriwa kwa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- 4.5 Makubaliano pamoja na masharti ya upangaji ni lazima yafuatwe na mpangaji vinginevyo Mkataba huu utavunjwa na Mwenye Kiwanja muda wowote.
- 4.5 Mkataba huu utakuwa kwa lugha ya Kiswahili na utakuwa katika nakala halisi Tatu (3).

KWA USHUHUDA BASI, pande zote mbili zinazohusika katika Mkataba huu zimeweka saini zao hapa chini kama ifuatavyo:-

Mkataba huu umewekwa saini na kupokelewa na
CRISPIN MUTABUZI MUSHUMBUSI ambaye namjua
 leo tarehe Mwezi 2024.



MWENYE BOHARI

MBELE YA

JINA: AGNES DOMINICK

CHEO: EDUWHA VIAPU WAKIL

ANWANI: 78857 DSM

SAHIHI: Agnes Dominick



Mkataba huu umewekwa saini na kuwekwa LAKIRI
 Na **BUFFALO BICYCLE TANZANIA**
 leo tarehe.....mwezi 2024.



MPANGAJI

MBELE YA

JINA: MAUREEN KOLENYO

CHEO: REGIONAL DIRECTOR - EA

ANWANI: IT PLAZA BUILDING 1ST FLOOR SUITE

SAHIHI: Maureen Kolenyo

JINA: *Rayson Elstora Luka*

CHEO: *WAC LU*

ANWANI: *P. O - Box 72015 DG*

SAHIHI: *[Signature]*

